




Nilisikia, "Hodi! Hodi!"



"Ni nani, jamani?"
Niliuliza huku
nikisinzia.



"Ni mimi." Sauti
inayokwaruza sikio
ilinijibu.



"Nani ndiye 'Mimi'?"
Niliuliza.



"Nilikwambia kuwa, ni-mi-mi tu." Sauti ile ile ilisema.



Niliajibu, "Mimi sijui
mtu ye yote anayeitwa,
'ni-mimi tu.'"

Nilitazama ikiwa
chandarua changu
kilikuwa kimenikinga
vizuri.



"Jina langu ni Amosi."
Sauti iliyokwaruza
zaidi kuliko awali
ilisema.

Ilisikika ikiwa karibu
sana na sikio langu.




"Amosi nani?" Niliuliza
huku nikitazama ndani
ya chandarua.



Kuito." Hatimaye, sauti
ilisema. Wakati huo
huo niliumwa sikioni.



"Uui!" Niliruka juu na
kuondoka kitandani.
"Utalipia kitendo hiki!"
Nilipiga kelele.



Kwa hasira, niliiasha
taa kumtafuta adui
wangu.



Nilitangaza vita dhidi
ya Amosi Kuito
msumbufu!